



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA ITIGI
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)



Kumb. Na. HW/ITG/F2/6/ 55

15 Octoba, 2024.

WANANCHI WOTE,
HALMASHAURI YA WILAYA YA ITIGI.

Yah: TANGAZO LA KAZI ZA MKATABA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Itigi anawatangazia wananchi wote wenye sifa nafasi za kazi (11) za wafanya usafi wa Mazingira na Udhibiti wa Taka. Waombaji wa nafasi hizo wawasilishe maombi yao ya kazi kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Itigi kwa kuzingatia vigezo na maelekezo kama ilivyo katika tangazo hili.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Itigi anawatangazia wananchi wote wenye sifa zinazotakiwa kujaza nafasi 11 za ajira ya mkataba kwa kazi ya kufanya usafi na Udhibiti wa taka. Nafasi za kazi zinazotangazwa ni zifuatazo:-

1. Nafasi za usafi wa mazingira stendi ya Rungwa 3
2. Nafasi za usafi wa Mazingira maeneo ya Umma Itigi 6
3. Usafi wa Mazingira maeneo ya machinjio ya Itigi na Mitundu 2

1.0 SIFA ZA MWOMBAJI

- ❖ Awe raia wa Tanzania
- ❖ Awe na umri kati ya miaka 18 na 65
- ❖ Awe na elimu kuanzia darasa la saba na kuendelea
- ❖ Awe anajua kusoma na kuandika kwa lugha ya Kishwahili
- ❖ Awe mwenye afya njema
- ❖ Awe mchapakazi na mwenye kujituma
- ❖ Awe mwenye nidhamu ya kazi
- ❖ Awe na utayari wa kufanya kazi kwa muda usiopungua masaa nane(8) kwa siku
- ❖ Awe ni mkazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Itigi